



**Kuna njia nyingine.**

**Mkutano wa Suluhisho  
Uwezeshaji (RMF)**  
husaidia wazazi na  
walimu kuzingatia  
mahitaji ya mwanafunzi.

**Msaидизи алиевнзуа**  
хуфана кази на wahusika  
воте кутатua mizozo,  
ambayo inaweza kuondoa  
hitaji la kuendelea na kesi.



**OFFICE FOR DISPUTE RESOLUTION**  
6340 Flank Drive  
Harrisburg, PA 17112-2764

**TUPIGIE SIMU ...**  
(800) 222-3353      (717) 901-2145  
WATUMIAJI WA TTY: PA Relay 711

**TUTEMBELEE KWENYE WAVUTI ...**  
[www.odr-pa.org](http://www.odr-pa.org)




Kupitia Ofisi ya Kutatua Mizozo, Idara ya Elimu ya Pennsylvania (PDE) inatimiza wajibu wake wa kisheria wa kudumisha mfumo wa mchakato wa elimu maalum. PDE inaaifikiana na Kitengo cha Kati cha Susquehanna ili kutoa usaidizi wa kifedha na usimamizi fulani kwa ofisi hiyo, bila kuhusika katika shughuli kubwa.

Kitengo cha Kati cha Susquehanna (CSIU) hakitabagua katika mpango wa elimu, shughuli au mazoeya ya uajiri kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, ulemauvu, hali ya ndoa, umri, dini, uelekezo wa kingono, ukoo, uanachama wa chama au uainishaji mwagine unaolindwa kisheria. Tangazo la sera hii ni kwa mujibu wa Kichwa cha VI cha Sheria ya Haki za Kiraia ya 1964, Title IX ya Marekebisho ya Elimu ya 1972, Sehemu ya 504 ya Sheria ya Urekebishaji ya 1973, na Sheria ya Wamarekani Wenye Ulemauvu ya 1990. Wafanyakazi na washiriki wa mpango ambao wana maswali au malamikyo ya watu wenye ulemauvu, wanapaswa kuwasiliana na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, CSIU, 90 Lawton Lane, Milton, PA 17847; (570) 523-1155.

**OFISI YA  
UTATUZI WA MZOZO**

**Uwezeshaji wa  
Mkutano wa  
Utatuzi**



**Njia mbadala  
ya kutatua  
kutokubaliana kuhusu  
elimu maalum**

## RMF ni nini?

**Mkutano wa Utatuzi** unahitajika kwa maombi kesi yanayoanzishwa na wazazi, isipokuwa wahusika wote wakubali kujaribu upatanishi.

Usikilizaji wa kesi unapoombwa, kuna mzozo, na wahusika wote wanaweza kuwa na ugumu wa kufikia makubaliano katika mkutano wa utatuzi. Kuwepo kwa **msaidizi asiyependelea** upande wowote katika mkutano wa utatuzi kunaweza kusababisha mkutano wa ufanisi zaidi.

Ikiwa wahusika wote wanaamini kuwa matumizi ya mhusika mwagine asiyependelea upande wowote yataongeza uwezekano wa kufikia makubaliano, **ODR itatuma msaidizi baada ya ombi**.

## Faida za RMF ni zipi?

### Uvezeshaji wa Mkutano wa Utatuzi (RMF) umeundwa ili ...

- Kuunda na uboresha uhusiano kati ya wazazi na walimu
- Kutoa fursa kwa wahusika wote kutatua migogoros
- Kuhimiza wazazi na walimu kutambua chaguo mpya za kushughulikia maswala ambayo hayajatatuliwa
- Kuunda mkutano usio na mkazo
- Kusaidia wahusika wote kushiriki kikamilifu
- Kutoa fursa ya kusuluhiha maswala na kutoa hitaji la kuendelea na kesi

## Ni nani anayeweza kuomba RMF?

Aidha mzazi au mfanyakazi wa shule (shirika la elimu la mtaa) anaweza kuomba **Uvezeshaji wa Mkutano ya Utatuzi (RMF)**. Hata hivyo, lazima wahusika wote wakubali kujumuisha msaidizi katika Mkutano wa Utatuzi, kwa sababu ni mchakato wa hiari.

## RMF hufanyika lini?

Kulingana na sheria, lazima Mkutano wa Utatuzi ufanyike ndani ya siku 15 baada ya ombi la kesi. Hata hivyo, ili kutoa kila fursa ya makubaliano, ODR itatuma msaidizi hadi **siku 30** baada ya ombi la kesi kupokelewa.

## Kuna gharama ya RMF?

**Hakuna gharama** kwa mhusika ye yote - wazazi au walimu - kwa kutumia Msaidizi wa Mkutano wa Utatuzi. RMF hailipishwi.



## Mchakato wa RMF huanzaje?

Wazazi na walimu wanapokubaliana kuhusu **tarehe, saa na eneo** la Mkutano wa Utatuzi, na wamekubali kutumia **msaidizi** ODR inaweza kupatikana.

Ombi la RMF likipokewa, ODR humtuma msaidizi kuhudhuria mkutano.

Katika mkutano huu, msaidizi atawaomba wahusika watie saini kwenye fomu inayoonyesha makubaliano yao ya msaidizi kuwepo.

## Jukumu la msaidizi ni nini?

### Msaidizi ...

- Husaidia wahusika kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi
- Husaidia wahusika kusuluhiha kutokubaliana kunakotokea wakati wa mkutano
- Hutoa mifano ya mawasiliano na usikivu mzuri
- Hudumisha mawasiliano wazi kati ya wahusika wote
- Hudumisha kutokuwa na upendeleo na haungi mkono upande wowote, kutoa lawama au kuamua ikiwa uamuzi fulani ni sawa au si sawa
- Hufafanua mambo ya makubaliano, lakini haitoi uamuzi kwa kikundi